

5. Vituo vya afya ya jamii

Huduma ya afya ya umma

Huduma hizi hulenga kulinda afya, kuzuia maradhi, magonjwa na majeraha na kukuza afya na usalama.

Huduma ya pombe, tubako na madawa mengine

- matibabu, usaidizi na maelezo, na mipango ya uzuiasi (kuepuksana)

Huduma ya kuchunguza kansa

- Mipango ya uchunguzi wa kansa ya matiti na kansa ya mlango wa kizazi

Mipango ya Matangazo ya Afya

- Kampeni ya matangazo ya afya ili kuhutubia masuala ya kipaumbele ya kiafya pamoja na chakula, shughuli za kimwili, uzuiasi majeraha na kujikinga na juu

Mipango ya Kusimamia Mtindo wa maisha

- Elimu ya mtindo wa maisha yenye afya na huduma za afya kwa kuzingatia usimamizi wa kibinafsi wa magonjwa ya kurithi kama yabisi, ugonjwa wa sukari, hali ya mfumo wa kupumua, unene sana na magonjwa ya mifupa

Huduma za afya ya ngono

- Kliniki za afya ya ngono, wauguzi wa afya ya wanawake na kampeni ya elimu ya afya ya ngono

Mipango ya afya na vikundi vya usaidizi

Vituo vingi vya afya ya jamii hutoa vikundi vya usaidizi na mipango ya kujisaidia binafsi kwa watu wenyewe magonjwa maalumu. Mifano ni pamoja na:

- Mpango wa Yabisu wa Kujisaidia binafsi
- Vipindi vya Elimu ya Pumu
- Mpango wa Urudishaji Mapigo ya moyo
- Darasa la upishi mara moja au mbili
- Maelezo ya Afya Nyumbani
- Mpango wa Uwepesi (upunguzo wa uzito)
- Kikundi cha Kuwasaidia Wagonjwa wa Sukari
- Matembezi ya Duka kuu

Wasiliana na kituo cha afya ya jamii cha mtaa wako kuhusu maelezo ya mipango na vikundi vinavyopatikana.



Wakalimani

- Una haki ya mkalimani mtaalamu ikiwa unahitaji mmoja unapokuwa ukitumia huduma ya Queensland ya afya ya umma
- Wakalimani wanaweza kupeanwa aidha ana kwa ana au kwa simu bila malipo
- ni sera ya afya ya Queensland kutumia marafiki na jamaa wakati wa hali za dharura tu. Ikiwa rafiki au jamaa yuko chini ya umri wa miaka 18 hastahili kutumiwa kama mkalimani kwa hali yeoyote ile
- tafadhal ikiwa unahitaji mkalimani, uliza mapema ili mipango ya miadi yako iweze kufanywa..

Karatasi hii ya kweli iko katika mfululizo wa 10. idadi kamili:

1. Mfumo wa afya nchini Queensland
2. Kumwona daktari
3. Madawa
4. Hospitali za Queensland
5. Vituo vya afya ya jamii
6. Huduma za meno
7. Afya ya pamoja
8. Kuishi na afya na kuzuia magonjwa
9. Huduma za afya na usaidizi kwa vikundi maalumu
10. Wewe na mfumo wa huduma ya afya